

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA

25 JUNI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA THELATHINI NA SITA – TAREHE 25 JUNI, 2015

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA:

Hati za Uhamishaji Fedha Na. 1 na Na. 2 za Mwaka wa Fedha 2014/2015 (*Statement of Reallocation Warrant No 1 and No 2 for the financial Year 2014/2015*)

II. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

255. MHESHIMIWA DKT. HENRY DAFFA SHEKIFU (LUSHOTO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Serikali iliahidi kusaidia kulipa gharama za usanifu wa mradi wa maji kwa Kata za Malibwi, Kwehanga na Kilole (Water Supply Project):-

- (a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kukamilisha zoezi hilo la kulipa gharama za Usanifu hatimaye Ramani zikamilike;
- (b) Je, Serikali itasaidiaje katika kutekeleza Mradi huo kama Usanifu umekamilika.

256. MHESHIMIWA MCH. LUCKSON NDAGA MWANJALE (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati Vijijini.

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

257. MHESHIMIWA MARGARETH AGNESS MKANGA (VITI MAALUMU)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Inasemekana kuwa mkojo wa popo umebeba virusi vinavyoambukiza ugonjwa wa EBOLA:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hili na inalifahamu;
- (b) Kama inalifahamu, Je ni utaratibu gani unaotumika kuangamiza popo hapa nchini.

WIZARA YA UJENZI:

258. MHESHIMIWA SAID AMOUR ARFI (MPANDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-
Miundombinu ni muhimu sana katika
kuunganisha nchi na kuharakisha maendeleo:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya lami ya
kuunganisha Wilaya ya Mpanda, Mlela,
Sikonge na Tabora.

WIZARA YA FEDHA:

259. MHESHIMIWA AMINA ABDULLA AMOUR (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-
Suala la matumizi ya mashine za EFD kwa
wafanyabiashara nchini halikuwa na matokeo
yaliyotarajiwa kwa sababu wafanyabiashara
wengi wanakataa kutumia mashine hizo:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi
wa kuhakikisha mashine hizo zinafanya
kazi;
- (b) Je, kufukuzana na wafanyabiashara na
kuwakamata viongozi wao ndiyo suluhisho
sahihi kwa tatizo hilo.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge zima
na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2015 [*The
Finance Bill, 2015*]

IV. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI

**DODOMA
25 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**